HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHESHIMIWA ZELOTE STEPHEN ZELOTE WAKATI WA KUMKABIDHI MWENGE WA UHURU 2017 MHESHIMIWA MKUU WA MKOA WA SONGWE KATIKA KIJIJI CHA MKUTANO, WILAYANI MOMBA MKOA WA SONGWE TAREHE 11 APRILI, 2017

Mheshimiwa Luteni (Mstaafu) Chiku Gallawa Mkuu wa Mkoa wa Songwe,

Ndugu Amour Hamad Amour, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, 2017

Ndugu Wakimbiza Mwenge Kitaifa,

Ndugu Wakufunzi wa Wakimbiza Mwenge Kitaifa, 2017

Ndugu Wenyeviti wa CCM Mkoa wa Rukwa na Songwe,

Ndugu Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa wa Rukwa na Songwe,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya Kutoka Mikoa ya Rukwa na Songwe,

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Ndugu Wanahabari,

Ndugu Wananchi,

Mabibi na Mabwana.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Kabla ya jambo lolote ni vyema kwa pamoja tumshukuru Mola wetu aliyetulinda na kutukutanisha pamoja.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kumlinda Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017 Ndugu **Amour Hamad Amour** pamoja timu nzima ya Wakimbiza Mwenge bila kuwasahau wakufunzi wao wawili Ndugu **Julius Shulla Tweneshe** na Ndugu **Khatibu Haji Khardi.** Wote kwa pamoja tuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu awalinde na kuwaweka

katika afya njema katika jukumu hili muhimu walilokabidhiwa na Taifa.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa

Hapa katika eneo hili la Mkutano kama linavyoitwa; tumekutana kwa sababu moja kubwa nayo ni kukabidhi Mwenge wa Uhuru 2017 na itifaki yake kwa Mkoa wako wa Songwe. Kabla ya kufanya hivyo ninayo mambo machache ya kuzungumzia.

Kwanza, tumepokea Mwenge wa Uhuru 2017, Kiongozi wa Mbio za Mwenge na Wakimbiza Mwenge Kitaifa jumla yao wakiwa sita na Wakufunzi wao wawili tarehe 07 Aprili, 2017 ukitokea Mkoa wa Katavi ukiwa salama, unawaka, unang'ara na unameremeta.

Pili, Wakimbiza Mwenge wote walikuwa salama na wenye afya njema wakiwepo wakufunzi wao. Ndani ya Mkoa wa Rukwa mambo hayo mawili

yalisimamiwa kwa kiwango cha hali ya juu sana bila kusahau itifaki zote za Mwenge.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa

Mwenge wa Uhuru 2017 katika Mkoa wa Rukwa umefanya kazi kubwa ya kuwafahamisha na kuwahamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kutimiza azma ya Serikali kwa Kauli mbiu isemayo:-

"Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu", na uhamasishaji katika:

Mapambano dhidi ya Rushwa, Mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevya, Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI na Mapambano dhidi ya Malaria.

Napenda nikuhakikishie ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017 uliotolewa katika Mkoa wa Rukwa umepokelewa na Wananchi kwa hamasa kubwa jambo ambalo tunaamini litaleta mabadiliko chanya kwa jamii Mkoani kwetu.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa

Mwenge wa Uhuru 2017 umekimbizwa katika Halmashauri Nne zilizopo katika Wilaya Tatu za Mkoa wa Rukwa. Halmashauri hizo ni; Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Halmashauri ya Wilaya Kalambo, Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Mbio hizo zimechukua umbali wa takribani Kilometa 749.2 ukitembelea miradi 43 katika mchanganuo ufuatao:-

Sekta ya Elimu 9, Afya 6, Maji 3, Miundombinu 2, Maliasili 5, Kilimo 4, Mifugo 4, Biashara na viwanda 5 na vikundi 24; (Vijana 13, Wanawake 6, Kikundi mchanganyiko 1, Kupambana na Dawa za kulevya 1 na Rushwa 3). Thamani ya miradi hiyo yote ni Shilingi 11,793,501,591.00.

Shughuli zilizofanyika katika miradi hiyo ni pamoja na kuweka mawe ya msingi, kukagua, kuzindua na mingine kufunguliwa.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Mchanganuo wa uchangiaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

a) Wananchi wamechangia jumla ya **Sh. 1,545,666,600.00** sawa na asilimia **13.11** ya gharama zote
b) Halmashauri zimechangia **Sh. 817,246,745.00** sawa na asilimia **6.93**
c) Serikali Kuu imechangia **Sh. 7,796,894,763.00** sawa na asilimia **66.11**
d) Wadau wengine wamechangia **Sh.1,633,693,483.00** sawa na asilimia **13.85**

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wote katika Mkoa wa Rukwa walioshiriki kwa namna yoyote ile kuhakikisha kwamba Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017 zinafanikiwa na kwa kweli zimefanikiwa. Tutaendelea kuenzi Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa

ambao unaleta matumaini pasipo na matumaini, upendo mahali palipo na chuki na heshima palipo na dharau.

Wito wangu kwa wananchi wote wa Rukwa kazi kubwa ambayo Mwenge wa Uhuru 2017 umeifanya katika Mkoa wetu ni mtaji ambao tunapaswa kuutumia kuleta maendeleo ndani ya Mkoa na hasa la viwanda jambo ambalo linawezekana kwa kuwa ni Mkoa wa uzalishaji mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wakimbiza Mwenge Kitaifa 2017 chini ya Kiongozi wao shupavu, msomi mzuri, muungwana, mwelewa, mwenye ushauri Ndugu **Amour Hamad Amour.** Chini yake anao vijana mahiri, wakakamavu wanaojituma kweli kweli. Nidhamu yao ni ya hali ya juu. Hawana makuu, wasikivu na wenye kujali na kushirikiana na kila mtu. Naamini haya ni matunda ya kazi nzuri

wanayoifanya wakufunzi Ndugu Julius Shulla Tweneshe na Ndugu Khatib Haji Khardi, tunawapongeza sana.

Katika kipindi cha siku nne wamefanya kazi yao kwa ujasiri, ukakamavu na ushirikiano usio na mfano; tutawakumbuka sana. Napenda niwahakikishie njia pekee ya kuwaenzi katika Mkoa wa Rukwa ni kutafsiri kwa vitendo yote waliyotufahamisha na kutuhamasisha kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Natambua ukiwa ni jirani yangu Mkoa wako una changamoto nyingi kwa kuwa ni Mkoa mpya. Vijana hawa kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017 naamini watafanya kazi nzuri sana kupitia kauli mbiu: ***"Shiriki kukuza uchumi wa Viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu".*** Nina uhakika watakuachia mtaji wa kutosha kwa ajili ya Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Maneno yangu hayatakamilika kama sitatoa pongezi kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa namna walivyoshikamana na kushiriki kwa namna mbalimbali kufanikisha Mbio za Mwenge Kitaifa katika maeneo yaliyofikiwa. Natambua wengi walipenda kufikiwa na Mbio hizo lakini hawakubahatika. Nawaomba wawe na subira kwa mwaka ujao watafikiwa.

Nawashukuru Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Halmashauri zote, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Madereva, Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini, Vijana wa skauti, Vikundi vya Hamasa na Burudani, Waandishi wa Habari bila kusahau Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na zile za Wilaya kwa ushirikiano uliokuwepo katika Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2017 katika Mkoa wa Rukwa. Asanteni sana.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Sasa tunakuja katika hatua ngumu. Hapa tulipo machozi yanatulenga. Kuagana na kuachana huwa ni jambo gumu na hasa kuachana na vijana kama hawa ambao wameacha alama na kukumbuka kazi nzuri katika Mkoa wa Rukwa. Napenda niseme toka moyoni mwangu kwa dhati kabisa tunawapenda sana tungependa kubaki nao japo hata tukavune nao mavuno ya msimu tunaotegemea hivi karibuni nao msimu huu.

Kwa kuwa haiwezekani nataka tuwaage LAKINI niwaombe wakumbuke Rukwa; mara wamalizapo jukumu hili walilopewa na Taifa.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Naomba sasa nikukabidhi Wakimbiza Mwenge Kitaifa 6 pamoja na Wakufunzi kama ifuatavyo:-

1) Ndugu **Julius Shulla Tweneshe** Kutoka Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu

2) Ndugu **Khatibu Haji Khardi** kutoka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto – Zanzibar

3) Ndugu **Salome Obadia Mwakitalima** Kutoka Mkoa wa Katavi

4) Ndugu **Fredrick Joseph Ndahani** Kutoka Mkoa wa Singida

5) Ndugu **Vatima Yunusu Hassan** Kutoka Mkoa wa Kusini Pemba

6) Ndugu **Bahati Mwaniguta Lugodisha** kutoka Mkoa wa Geita

7) Ndugu **Shukrani Islam Msuri** Kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi

8) Ndugu **Amour Hamad Amour** Kiongozi wa Mbio za Mwenge 2017 kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Sasa nichukue fursa hii kukukabidhi rasmi Mwenge wa uhuru ukiwa unang'ara, unameremeta na ukiwa salama salimini.

Mwenge Hoyeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!

Rukwa Hoyeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!!

Songwe Hoyeeeeeee!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!

Asanteni kwa kunisikiliza.